HARAMBEE

JAMUHURI YA KENYA

# SERA YA MASUALA YA KIGENI YA JAMHURI YA KENYA





NAKALA FINYU

# SERA YA MASUALA YA KIGENI YA JAMHURI YA KENYA

## NAKALA FINYU

©Serikali ya Kenya 2024. Haki Miliki zote Zimehifadhiwa

# YALIYOMO

UTANGULIZI........................................................................ iii

DIBAJI........................................................................ iv

SHUKRANI........................................................................ v

RAMANI YA KAUNTI ZA KENYA........................................ vi

VIFUPISHO........................................................................ vii

IKISIRI........................................................................ x

*Sura ya 1*: **MUKTADHA WA USULI**.................................................... **1**

**1.1 Muktadha wa Sera na Sababu**........................................ **1**

**1.2 Sera ya Masuala ya Kigeni na Matakwa ya Taifa**.......... **1**

**1.2.1 Kipaumbele cha Matakwa ya Taifa**............................ **1**

**1.2.2 Mitazamo Kiini**........................................................ **2**

**1.2.3 Maadili ya Taifa**........................................................ **2**

**1.3 Malengo ya Sera ya Masuala ya Kigeni**......................... **2**

**1.4 Agenda Badilishi ya Kitaifa kutoka 2022 na kuendelea** **2**

*Sura ya 2:* **MAZINGIRA FANYIZI**.................................................... **4**

**2.1 Mazingira ya Nchini na Nje ya Nchi**............................ **4**

**2.2 Mawanda ya Wahusika katika Sera ya Masuala ya Kigeni** **4**

**2.3 Matumizi ya Ushawishi (Diplomacy) wa Umma**.......... **5**

*Sura ya 3:* **USHAWISHI JOZI NA WINGI**........................................ **6**

**3.1 Ufafanuzi wa Ushawishi Jirani** ...................................... **6**

**3.2 Ushirikiano na Mataifa ya Kiafrika**............................... **6**

**3.3 Ushirikiano na Ulimwengu Wote**.................................. **7**

**3.4 Ushawishi Mwingi**........................................................ **7**

3.5 Sera ya Masuala ya Kigeni na Makundi Shirikiano jumui na madogo........................................................................... 8

3.6 Mabadiliko ya Nairobi kama Kitovu cha Ushirikiano Jumui na Fedha........................................................................... 8

*Sura ya 4:* SERA YA KENYA YA MASUALA YA KIGENI: MAENEO LENGWA............................................................... 9

4.1 Maeneo Lengwa Manane.................................................. 9

4.2 Ushirikiano wa Amani na Usalama................................ 10

4.3 Ushirikiano wa Kiuchumi na Biashara.......................... 10

4.4 Bahari na Ushirikiano baharini (blue)........................... 12

4.5 Utawala wa Ulimwengu na Ushirikiano jumui............. 12

4.6 Mazingira na Ushirikiano wa Tabianchi....................... 13

4.7 Ushirikiano wa Sayansi, Teknolojia na Uvumbuzi........ 13

4.8 Ushirikiano wa Wakenya nje ya Nchi............................ 14

4.9 Ushirikiano wa Jamii na Utamaduni.............................. 15

*Sura ya 5:* MPANGILIO WA UTENDAJI WA TAASISI..................... 16

5.1 Jukumu la Sekretariati ya Serikali................................. 16

*Sura ya 6:* UFUATILIZI NA UTATHMINI.......................................... 19

6.1 Umuhimu wa kupima Matokeo ya Ushirikiano............ 19

# UTANGULIZI



Sera ya masuala ya Kigeni ya Kenya na ushirikiano wa kidiploma sia lazima uwe uchochezi wa kuboresha riziki na maisha ya kila Mkenya na kusukuma mbele maendeleo na ustawi wa taifa katika ulingo wa ulimwengu. Sera hii ya Masuala ya Kigeni 2024 kama inayoelezwa hapa ndani inawasilisha mpangilio mpana, elezi na fafanuzi kuendesha uhusiano wetu wa masuala ya kigeni na ushirikiano wa kidiplomasia. Kwa kujikita katika mtazamo wa kina wa mabadiliko ya uhusiano wa Kenya wenye washirika wengi, sera hii inaelekeza mkakati mahususi wa Kenya wa matakwa ya kitaifa katika muktadha wa mabadiliko daima ya Nyanja za kisiasa na kiuchumi.

Matokeo ni kuboresha Sera ya Masuala ya Kigeni ambayo bado imejikita katika kujitolea kwa dhati kuwasilisha, kuendeleza na kulinda matakwa na sura ya taifa ulimwenguni, itapa ta kichocheo bora kutoka kwa serikali yangu yenye lengo kusudio la kuinua msimamo wa Kenya katika jamii ya mataifa, kupitia mkabala wa mustakabali na uvumbuzi wa diplomasia.

Toleo hili la Sera ya Masuala ya Kigeni inafafanua msimamo wa Kenya wa dhati kutoa ki paumbele kwa muungano wa maeneo, kuimarisha ushirikiano wa Afrika kuinua mtazamo mpya wa upendo wa Afrika, hata tunapoendelea kuimarisha na kupanua muonekano wetu wa nchi ulimwenguni.

Uteuzi huu makinifu wa malengo yetu ya Sera ya Masuala ya Kigeni unachochewa na kutaka taifa la amani, umoja na linalonawiri, kama ilivyowekwa katika Katiba ya Kenya; Wimbo wa Taifa, na maandiko ya sera ya muda mrefu. Maeneo lengwa mahususi yatakayofuatili wa na serikali yangu yakiongozwa na sera hii, kweli yanaakisi kujitolea kwetu kukabiliana kwa ubunifu maswala mapya na ibuka ulimwenguni, hivyo kulenga maeneo mapya hayo ambayo yako nje ya maswala asili ya kidiplomasia yakijumuisha dijitali na teknolojia, tabianchi, afya na mabadiliko ya Kiutawala ya Ulimwengu. Pia kuelekeza upya makabiliano kwa tishio jipya la amani na usalama.

Utekelezaji fanisi wa Sera hii ya Maswala ya Kigeni unahitaji mkabala thabiti na wenye uta tibu bora unaojumuisha sekta zote; kutoka serikalini kupitia “Mkabala wa Serikali Yote”, sekta ya Kibinafsi na Washirika nje ya Nchi yetu. Ni matarajio yangu kwamba wizara zote za serikali, idara, mashirika na vitengo faafu vitafanya kazi kwa karibu na Wizara ya Masuala ya Kigeni na Diplomasia kutekeleza maono ya sera hii ya Maswala ya Kigeni.



**MHESHIMIWA, DKT. WILLIAM SAMOEI RUTO PhD, C.G.H**
**RAIS WA JAMUHURI YA KENYA**

# DIBAJI



Wizara ya Masuala ya Kigeni na Wakenya walio nchi za kigeni, imepewa jukumu la kusimamia Sera ya Masuala ya Kigeni na kufikia malengo ya kulinda, kuendeleza na kufafanua matakwa ya taifa. Mara ya kwanza Kenya ilichapisha Sera jumla yake ya Masuala ya Kigeni mwaka wa 2014. Kutoka wakati huo, tumeona mabadiliko makubwa katika mazingira ya ulimwengu. Matakwa ya Kenya ya kitaifa yamepanuka kwa mapana na kukua kama nchi yetu inasaka jukumu mahususi katika masuala ya kimataifa, na kuweka Kenya kama kitovu cha kimataifa. Ili kukabiliana na matakwa hayo, Wizara imepitia mageuzi makubwa, na lengo la jumla la kuongeza utarazaki katika kiwango cha kidiplomasia na kuwezesha vituo vyetu vya kigeni kuchukuwa jukumu kubwa hisitahiki katika kuendeleza sera yetu ya maswala ya kigeni na maendeleo ya taifa.

Upanuzi wa mwelekeo wa kidiplomasia wa Kenya na utambuzi wa jukumu la wanawake na vijana katika diplomasia, unaendelea kustawisha Sera yetu ya Masuala ya Kigeni. Uhakiki wa Sera yetu ya Masuala ya Kigeni unaakisi uhalisia wa sasa wa hapa nyumbani na kimataifa, na kuhakikisha inabaki kuwa fafau na kulenga mustakabali wetu unaotosha kwa lengo na kuendeleza matakwa ya taifa la Kenya.

Historia ya kidiplomasia ya Kenya inakubali kwa dhati jukumu la kuwa chonjo na hekima kamanchi mojawapo ya jamii ya kimataifa. Tumejenga kwa umakinifu, na kudhibiti uhusiano wa maelewano na changamfu na nchi jirani Afrika, na ulimwenguni kote kwa jumla. Maadili ya taifa, misimamo ya sera ya masuala ya kigeni na matakwa ziada ya taifa yanalazimisha uelezaji sahihi na utekelezaji. Fauka ya hayo, yanaelekeza mfumo wetu tunaothamini wa kuhushimu haki za kibinadamu, sera isiyo na ufisadi na utawala bora.

Katika kiini cha sera hii ya masuala ya kigeni, kuna maeneo lengwa muhimu juu ya Diplomasia yaAmani na Usalama; Diplomasia ya Uchumi na Biashara; Diplomasia ya Utawala Ulimwenguni na Uhusiano wa nchi nyingi; Diplomasia ya Mazingira na Tabianchi; Diplomasia ya Sayansi, Teknolojia na Uvumbuzi; Diplomasia ya Wakenya walio nchi za kigeni; na Diplomasia ya Utamaduni na Jamii.

Uhakiki wa Sera ya Masuala ya Kigeni ulifanyika kupitia mkabala kutafuta maoni na ushirikishi mpana kwa kuegeme masharti ya Katiba yetu. Sera hii inaendelea kuhakikiwa ili kuhakikisha ibaki faafu, inayofana na inayosikiliza katika kuendeleza matakwa na maadili yetu ya taifa. Tunatambua na

kupongeza ushirikiano na maoni ya wachangiaji, ambao mchango wao wa thamani zaidi ulijenga maono ya sera hii ya masuala ya kigeni inayojumuisha matarajio ya Kenya na kuiweka nchi hii kupata nafasi ibuka kwa maendeleo endelezi na usitawi.



MHESHIMIWA DKT. MUSALIA MUDAVADI, E.G.H
WAZIRI MKUU WA BARAZA LA MAWAZIRI NA WAZIRI WA MASWALA YA KIGENI NA WAKENYA WALIO NCHI ZA KIGENI

# SHUKRANI



Mwaka jana wote, Wizara ya Masuala ya Kigeni na Wakenya katika Nchi za Kigeni ikishirikiana na Idara za Serikali na washikadau walifanya uhakiki mpana wa Sera ya Masuala ya Kigeni. Uhakiki huu ulinuia kuhakikisha kuwa sera hii ni kakamavu katika kushughulikia majukumu mawili ya kulinda matakwa yetu yote ya kitaifa na vipaumbele vya maendeleo, huku ikihakikisha sura ya Kenya kama memba mwajibikaji wa jamii ya kimataifa.

Katika mchakato huu wa kupitia upya sera hii, tuliangazia ufanisi wetu, tathmini ya jicho la ndani, mikabala yetu iliyopo kwa sasa, na tukaona mustakabali wa Kenya kunawiri na kuongoza katika ulingo wa ulimwengu. Mijadala ilifanyika na washikadau tofauti tofauti, kwa kuzingatia masharti ya katiba yetu ya kushirikisha umma na washikadau, tulichunguza sifa ambazo zina uzito katika kufuatiliza matakwa yetu ya kitaifa. Juhudi hizi zilidhamiria kujumuisha; mienendo ya kisiasa kimaeneo, utegemeano wa kiuchumi, maswala ya utamaduni na jamii, maendeleo ya kiteknolojia, maswala ya amani na usalama, pia matarajio ya utawala ulimwenguni, yote ambayo yanaongoza ushirikiano wetu ka tika masuala ya sasa ulimwenguni.

Utekelezaji faafu wa Sera hii ya Masuala ya Kigeni, utahitaji mkabala ratibu mpana unaojumuisha sekta zote- serikali, sekta ya kibinafsi, na washiriki wasio wa taifa letu. Kwa mtazamo huu, wizara, idara, mashirika na vitenge vya serikali vilivyo na majukumu ya masuala ya kigeni vina majukumu ya kufanya kazi kwa karibu na Wizara ya Masuala ya Kigeni na Wakenya katika Nchi za Kigeni, Toleo hili la Sera ya Masuala ya Kigeni, halingefaulubila ya kujitolea na jitihada kubwa ya watu wengi na taasisi za washikadau mbalimbali. Kwa niaba ya Idara ya Taifa ya Masuala ya Kigeni, kwanza natoa shukurani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Rais wa Jamuhuri ya Kenya na Waziri Mkuu akiwa vile vile Waziri wa Masuala ya Kigeni na Wakenya katika Nchi za Kigeni kwa kuongoza kwa busara mchakato huu wa kupitia upya na kuboresha sera hii.

Pili, nawashukuru kwa dhati washikadau wote kutoka vitengo mbalimbali, ikijumuisha kitengo cha Serikali Kuu, Baraza la Magavana, Seneti, Bunge la Taifa la Kenya, kitengo cha  ahakam ana Ofisi Huru za Kikatiba, Waheshimiwa Mabalozi wastaafu na wale waliomo kazini bado, sekta ya kibinafsi, Wasomi, mashirika ya kijamii, vijana na umma kwa jumla kwa michango yao mjarabu.

Mchango na mawazo yao yaliongoza njia mpya za ushurikiano na utendaji, ulizalisha mwako mpya wa ushirikiano na kurutubisha ufahamu wetu wa masuala yaliyopo.

Shukurani zetu aidha kwa Kamati ya Uhakiki ikiongozwa na Balozi Lucy Kiruthu, kwa kujitolea bila mipaka, kutayarisha na kutimiza ufanisi wa toleo hili la Sera ya Masuala ya Kigeni. Mchango wa wafanyikazi wa makao makuu ya Wizara na Balozi umekuwa wa thamani kubwa katika kurutubisha toleo hili. Mwisho, nawashukuru washirika wetu wote waliosaidia katika jukumu la kupitia upya na kuboresha sera hii kwa njia moja au nyingine. Asanteni sana nyote.



**DKT. A. KORIR SING'OEI**
**KATIBU MKUBWA, IDARA YA TAIFA YA MASUALA YA KIGENI**

# RAMANI YA KAUNTI ZA KENYA




| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 001 | Mombasa | 13 | Tharaka-Nithi | 25 | Samburu | 37 | Kakamega |
| 002 | Kwale | 14 | Embu | 26 | Trans-Nzoia | 38 | Vihiga |
| 003 | Kilifi | 15 | Kitui | 27 | Uasin Gishu | 39 | Bungoma |
| 004 | Tana River | 16 | Machakos | 28 | Elgeyo-Marakwet | 40 | Busia |
| 005 | Lamu | 17 | Makueni | 29 | Nandil | 41 | Siaya |
| 006 | Taita–Taveta | 18 | Nyandarua | 30 | Baringo | 42 | Kisumu |
| 007 | Garissa | 19 | Nyeri | 31 | Laikipia | 43 | Homa Bay |
| 008 | Wajir | 20 | Kirinyaga | 32 | Nakuru | 44 | Migori |
| 009 | Mandera | 21 | Murang'a | 33 | Narok | 45 | Kisi |
| 10 | Marsabit | 22 | Kiambu | 34 | Kajiado | 46 | Nyamira |
| 11 | Isiolo | 23 | Turkana | 35 | Kericho | 47 | Nairobi |
| 12 | Meru | 24 | West Pokot | 36 | Bomet | | |

# VIFUPISHO

**AMUMJ** - Agenda ya Mabadiliko ya Uchumi wa kuanzia Mshinani hadi Juu

**ATMIS** - Misheni ya Mpito ya Muungano wa Afrika nchini

**AZ** - Akili Zalishi

**BAW** - Bima ya Afya kwa Wote

**BBHJB** - Baraza la Bahari Hindi la Jinai Baharini

**BHSU** - Baraza Huru la Sayansi na Ushirikiano

**BMw** - Benki za Maendeleo wingi

**BNNK** - Biashara Ndogo Ndogo na za Kadri

**BNNK** - Biashara Ndogo Ndogo na za Kadri

**BUIUAK** - Brazil, Urusi, India, Uchina na Afrika Kusini

**BUUM** - Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa

**CKMAK** - Chama cha Kenya cha Mashirika Ajira ya Kibinafsi

**CMBH-UE** - Chama cha Mkondo wa Bahari Hindi cha Ushirikiano wa Eneo

**CMK** - Chama cha Mawasiliano ya Kimataifa

**CMRS** - Chifu wa Medali ya Roho Safi

**EBHA** - Eneo la Biashara Huru la Bara la Afrika

**EBHMM** - Eneo la Biashara Huru la Maeneo Matatu

**HFK** - Hazina ya Fedha ya Kimataifa

**HII** - Haramu, Isiyosemwa, Isiyosimamiwa

**HSsM** - Halimashauri ya Serikalishiriki juu ya Maendeleo

**HSsUM** - Halimashauri ya Serikalishiriki juu ya Ukame na Maendeleo

**HTS** - Hazina ya Tabianchi Salama

**HTU** - Huduma Tamba za Ubalozi

**JAM** - Jumuiya ya Afrika Mashariki

**JDC** - Jamuhuri ya Kidemokrasia ya Congo

**JKR** - PMUM- Jopo la Kimataifa la Raslimali

**JMK** - Jamii za Maeneo ya Kiuchumi

**JMKA** - Jumuia ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika

**JSKSsMWM**- Jukwaa la Sera ya Kisayansi ya Serikalishiriki ya Mimea na Wanyama na Mazingira

**JSsMT** - Jopo la Serikalishiriki la Mabadiliko ya Tabianchi

**KKEMM** - Kongamano la Kimataifa la Eneo la Maziwa Makuu

**KMAMT** - Kamati ya Marais wa Afrika wa Jamuhuri na Serikali juu ya Mabadiliko ya Tabianchi

**KMNV** - Kituo cha Mapinduzi ya Nne ya Viwanda

**KMU** - Kituo cha Mazingira Ulimwenguni

**KNFK** - Kituo cha Nairobi cha Fedha cha Kimataifa

**MAVM** - Msukumo wa Afrika wa Viwanda visivyoharibu Mazingira

**MBH** - Magharibi mwa Bahari ya Hindi

**MDAs** - Wizara, Idara na Mashirika

**Mh**. - Mheshimiwa (Rais)

**MIVMK** - Mpango IV wa Muhula Kadri

**MJTUU** - Mfumo Jumuishi wa Taifa wa Ufuatilizi na Utathmini

**MKB** - Mawasiliano ya Kanda za Baharini

**MKH** - Mahakama ya Kimataifa ya Haki

**MKJ** - Mahakama ya Kimataifa ya Jinai

**MMAS** - Misheni ya Muungano wa Afrika nchini Somalia

**MME** - Malengo ya Maendeleo Endelevu

**MMM** - Malengo ya Maendeleo ya Milenia

**MMRSK** - Mstahiki wa Medali ya Roho Safi ya Kenya

**MMw** - Mashirika la Mataifa wingi

**MSSM** - Misheni ya Usalama Saidizi ya Kimataifa

**MUM** - Mashirika ya Umoja wa Mataifa

**MUMUAD** - Misheni ya Umoja wa Mataifa na Umoja wa Afrika nchini Darfur

**MUMUC** - Misheni ya Umoja wa Mataifa ya Uimarishaji wa

**MUU** - Mkataba wa Uchumi Ushirikiano

**MUUPU** - Mashirika ya Ushirika wa Uwekaji Pesa na Utoaji Mikopo

**MVMM** - Mikutano, Vishawishi, Makongamano na Maonyesho/Matukio

**Mw** - Mashirika wingi ya Mazingira

**MwM** - Mkataba wa Maelewano

**MWS** - Mkabala Wote wa Serikali

**NIW** - Nchi Inayochanga Wanajeshi

**OUMMKU** - Ofisi ya Umoja wa Mataifa ya Madawa ya Kulevya na Uhalifu

**PMUM** - Programu ya Mazingira ya Umoja wa Mataifa

**PUMK** - Programu za Urekebishaji Miundo ya Kiuchumi

**RGW** - Reli ya Geji Wastani

**SHIRIKA** - Vitovu vya Uchumi wa Kijamii kwa Ujumuishaji wa Wakimbizi nchini Kenya

**SJMKA** - Soko Jumuia la Mashariki na Kusini mwa Afrika

**SKLK** - Shirika la Kimataifa Lisilo la Kiserikali

**SKMW** - Shirika la Kutofungamana na Mrengo Wowote

**SKV** - Shirika la Kilimo na Vyakula

**SKW** - Shirika la Kimataifa la Wafanyikazi

**SNACP** - Shirika la Nchi za Africa, Carribean na Pacific

**SNN** - Silaha Ndogo Ndogo

**SUA** - Shirika la Umoja wa Afrika

**SUMESU** - Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni

**SUSK** - Sekreteriati ya Utaratibu wa Serikali Kuu

**SUUK** - Shirika la Ujerumani la Ushirikiano wa Kimataifa

**TEKNOHAMA** - Teknolojia ya Habari na Mawasiliano

**TFMA** - Taasisi za Fedha za Muungano wa Afrika

**THUM** - Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka

**TS&U** - Teknolojia ya Sayansi na Uvumbuzi

**UBUK** _ Ushirikiano wa Biashara na Uwekezaji Kimkakati

**UKMM** - Uwekezaji wa Kigeni wa Moja kwa Moja

**UM** - Umoja wa Mataifa

**UPK** - Uhalifu Pangwa wa Kimataifa

**UTK** - Utalii na Turathi za Kitamaduni

**UU** - Ufuatilizi na Utathmini

**UU** - Umoja wa Ulaya

**UUK** - Ushirikiano wa Umma na Kibinafsi

**VAKKM** - Vituo vya Afrika vya Kudhibiti na Kuzuwia Magonjwa

**VVU** - Vikwazo Viso Ushuru

**WBM** - Waziri wa Baraza la Mawaziri

**WMK** - Wizara ya Masuala ya Kigeni

**ZJN** - Zao Jumla la Nchi

# IKISIRI

Toleo hili la Sera ya Masuala ya Kigeni linawakilisha matokeo ya kupitia upya Sera ya Masuala ya Kigeni ya Serikali ya Kenya. Mapito haya yalizingatia maoni na jitihada kutoka mchakato mpana wa ushirikiano wa kitaifa pamoja na washikadau muhimu, kwa kufuata maagizo ya Katiba yetu, jambo la lazima, juu ya kupata maoni ya umma. Sera hii imewakilishwa katika sura sita. Sura ya kwanza inaonyesha mukhtadha na mwendelezo wa Sera ya Masuala ya Kigeni ya Kenya. Sura hii zaidi, imejikita katika matakwa ya kitaifa ya Kenya, msingi ambao Sera yoyote ya masuala ya kigeni hujikita, pia inaonyesha mabadiliko ya Sera ya Masuala ya Kigeni ya Kenya tangu enzi za Ukoloni hadi uhuru na wakati wa sasa palipo na mabadiliko muhimu ya kiuchumi.

Sura ya pili inaonyesha mazingira ya utendaji, hususan masuala ibuka ya nchini na nje ya nchi ambayo yanaelekeza sera ya masuala ya kigeni ya Kenya. Nyongeza muhimu katika sura hii ni wahusika muhimu katika masuala ya kigeni tukikubali mabadiliko ya haraka ya hali hapa nyumbani na ulimwenguni. Wahusika hawa wanajumuisha, Raia, Bunge, CSOs, Vyombo vya Habari, Sekta ya Kibinafsi, Taasisi za Kidini, miongoni mwa wengine.

Katika Sura ya tatu, uhakiki umetekelezwa wa ushirikiano wa Kenya na mataifa mengine mengi, na kuweka msingi wan jia za kidiplomasia za Kenya. Ujirani wa kidiplomasia wa Kenya umeelezwa kwa kuonyesha 'ujirani wa kidiplomasia' wa karibu, ambao haurejelei tu Jumuia ya Afrika Mashariki (EAC) bali unapanuka hadi maeneo mengine ya kijografia ikijumuisha maeneo ya Mamlaka ya Serikalimseto juu ya Ukame na Maendeleo (IGAD). Sura hii pia inafafanua ushirikiano wa Kenya na Afrika yote na ulimwengu. Sura inaelezasifa za Kenya katika Diplomasia na mataifa mengi ikijumuisha sera ya nchi ya masuala ya kigeni kuelekea kwenye makundi mengi.

Sura ya nne, imejikita katika sehemu nane za Maeneo Lengwa ya sera ya masuala ya kigeni ya Kenya yakijumuisha Diplomasia ya Amani na Usalama; Diplomasia ya Uchumi na Biashara; Diplosia Makinifu na Bahari; Diplomasia ya Ushirikiano na Mataifa mengi na Utawala Ulimwenguni; Diplomasia ya Mazingira na Tabianchi. Nyingine ni: Diplomasia ya Teknolojia ya Kisayansi na Uvumbuzi; Diplomasia ya Wakenya nje ya nchi; na mwisho, Diplomasia ya Jamii na Utamaduni. Sura hii inaweka wazi malengo yakuzingatiwa chini ya maeneo lengwa ya kidiplomasia yaliyounganishwa kwa maelewano, na kulenga uteuzi wa kuyaweka maeneo ya kipaumbele ya Sera ya Masuala ya Kigeni ya Kenya.

Mwisho, toleo hili linaeleza katika Sura ya tano, mapendekezo ya mpangilio wa utekelezaji, kimsingi, 'Mkabala wa Serikali Yote na Jamii'. Sura ya mwisho inaeleza mpangiliokazi wa ufuatilizi na utathimini. Viababishi vinavyoleta ufuatilizi wa matakwa ya taifa la Kenya vinajumuisha: Diplomasia ya Siasa Kimaeneo, Utegemeano wa Kiuchumi na Ustawi, Maswala ya Kijamii na Kiutamduni, Maendeleo ya Teknolojia, Maswala ya amani na usalama, Matarajio ya utawala ulimwenguni.

## Mambo yanayoathiri mfuatilizo wa matakwa ya taifa la Kenya inajumuisha:

- Mifanyiko ya siasa kimaeneo.
- Utegemeano wa Kiuchumi na ustawi
- Maendeleo ya Kiteknolojia
- Maendeleo ya kiteknolojia
- Masuala ya amani na usalama
- Matarajio ya utawala wa ulimwengu



# Sura 1:

## 1.1 Mukhtadha wa Sera na Sababu

Sera ya Masuala ya Kigeni ni mpangiliokazi muhimu sana unaoeleza jinsi Kenya hutumia vifaa vya uwezo katika kufuatilia manufaa ya nchi na uzuri waulimwengu. Mpangilio makinifu wa muda mrefu wa maendeleo ya Kenya; Maono ya Kenya ya 2030; Agenda ya Mabadiliko ya Uchumi kuanzia Mashinani Kwenda Juu (BETA); na Mpango wa Nne wa Muda wa Kati (MTP IV) 2023-2027, unaweka Sera ya Masuala ya Kigeni kama kifaa cha maendeleo ya taifa.

Ongezeko la jukumu la teknolojia limefanya Diplomasia kuwa zaidi na zaidi shughuli ya umma, kuongezeka kwa ushiriki wa wahusika wasi wa taifa, ikijumuisha miongaoni mwa wengine, Sekta ya kibinafsi, mashirika ya jamii raia, Vyombo vya Habari na Mahakama. Ongezeko la ushirki wa umma unaenda sambamba na masharti ya Katiba ya Kenya inayoeleza ulazima wa ushiriki wa umma katika uundaji na utekelezaji wa sera.

## 1.2 Sera ya Masuala ya Kigeni na matakwa ya Taifa

Ibara 238 (1) ya Katiba ya Kenya inaeleza usalama wa taifa kuonyesha elementi kiini za manufaa ya kitaifa ya nchi. Uendelezaji na ulinzi wa manufaa haya ya Taifa ndiyo kiini cha Sera ya Masuala ya Kigeni ya Kenya. Katika Ibara 10 (1) na (2) maadili ya Kenya na mielekeo ya utawala ambayo ni muhimu katika kuendeleza umoja wa taifa, sifa za uraia, uzalendo, majivuno ya kitaifa na utaifa, yameelezwa.

### 1.2.1 Kipaumbele cha Matakwa ya Kitaifa

Matakwa ya taifa la Kenya yamepangwa kwa kigezo cha kipaumbele kwa mujibu wa umuhimu wake na athari ya maisha mema ya watu. Pia matakwa haya yanachukuliwa muhimu sana kwa ustawi wa nchi. Muonekano/sura ya uendelezaji na ulinzi wa matakwa haya na sura ya ulimwengu ni lengo muhimu la sera ya masuala ya kigeni ya Kenya. Kwa kufuatiliza haya, matakwa ya taifa yaliyopewa kipaumbele ni yafuatayo:

a) Heshima ya mipaka ya Taifa, Utawala bila kuingiliwa na Usalama wa Raia
b) Ustawi wa Kiuchumi
c) Uthabiti wa Kisiasa na Kijamii
d) Maadili na Utawala wa Taifa
e) Katiba na Uzingatifu wa sheria
f) Maendeleo Endelevu
g) Ushawishi na Ushinda wa Kilimwengu

### 1.2.2 Misimamo Kiini

Utekelezaji wa Sera ya Masuala ya Kigeni ya Kenya na ukabiliano na uhusiano wa kimataifa unaongozwa na misimamo ifuatayo:

i) Utaifa
ii) Ujirani mwema na kutoingilia masuala ya nchi nyingine
iii) Majimbo
iv) Upendo wa Afrika
v) Ubinadamu
vi) Urudishaji wema
vii) Kutoegemea mrengo wowote
viii) Ushirikiano na wanaofikiri kama sisi na mipangilio ibuka mingi

## 1.2.3 Maadili ya Taifa

Sera hii ya Masuala ya Kigeni inachochewa na maadili ya taifa na misimamo ya utawala kama yalivyowekwa katika Katiba ya Kenya, Ibara 10 (2). Maadili hayo ni yafuatayo:

i) Uzalendo, umoja wa taifa, ugavi na ugatuzi wa mamlaka, uongozi wa kuzingatia sheria, demokrasia, na ushiriki wa wananchi.
ii) Heshima ya binadamu, ujima, haki ya jamii, ujumuishaji, usawa, haki za binadamu, kutobaguwa na kulinda wale waliotengwa.
iii) Utawala mzuri, Heshima, uwazi na uwajibikaji, na
iv) Maendeleo endelevu

## 1.3 Malengo ya Sera ya Masuala ya Kigeni

Sera ya Masuala ya Kigeni ya Kenya inalenga kuongeza msimamo wa nchi kama kinara wa kanda na mtetezi faafu wa matakwa ya Afrika katika ulingo wa ulimwengu. Kufanikisha lengo hili, Sera hii ya Masuala ya Kigeni itafuatiliza malengo yafuatayo:

i) Kulinda uhuru na kuheshimu mipaka
ii) Kuendeleza amani na usalama katika rubaa za maeneo na ulimwengu
iii) Kusukuma mbele agenda ya nchi ya maendeleo na usitawi wa kiuchumi
iv) Kuweka Kenya katika nafasi ya uongozi wa udhibiti wa mazingira na tabianchi
v) Kuwasilisha, kuendeleza na kulinda sura na sifa ya nchi ulimwenguni
vi) Kuendeleza ushirikiano na mwingiliano wa eneo dogo nae neo makubwa
vii) Kuendeleza ushirikiano wa kimataifa, ushirikiano na mataifa mengi na kushiriki kwa vitendo katika utawala wa ulimwengu, na
viii) Kuongeza ushawishi wa Wakenya wanaoishi nchi za nje na kuendeleza, kulinda matakwa yao na maisha mazuri.

## 1.4 Agenda ya Mabadiliko ya Kitaifa kutoka 2022 na kuendelea

Tukiongozwa na maono ya Mheshimiwa Rais Dkt. William Samoei Ruto, Sera ya Kenya ya Masuala ya Kigeni imeendelea kuzingatia diplomasia ya Kiuchumi, kuishi kwa amani, jumuia ya eneo na umoja wa kimataifa kama wadhamini muhimu wa jukumu la uthabiti katika eneo. Manifesto ya utawala, Agenda ya Mabadiliko ya Kiuchumi kuanzia mashinani Kwenda juu (BETA)imelazi mu mabadiliko mengi katika mkakati wa kiuchumi na sera ya kigeni.



*Mheshimiwa Rais William Samoei Ruto, PhD, akihutubia Mkutano Mkuu wa Umoja wa Mataifa.*

*Sura* **2**:

# MAZINGIRA YA KUFANYA KAZI

## 2.1 Mazingira ya Ndani na Nje ya Nchi

Utaratibu na utendaji wa Sera ya Masuala ya Kigeni ya Kenya unaongozwa na mazingira ya nchini na yale ya nje ya nchi, maendeleo ya nchi, na wahusika wa taifa na wale wasio wa taifa. Wote hawa kwa pamoja, huathiri mkakati wa mkondo na matendo ya kidiplomasia ambayo yanafuatwa na nchi. Athari za nchini kwa pamoja hujenga na kuendeleza Sera ya Masuala ya Kigeni ya Kenya, kuyapanga pamoja na vipaumbele vya taifa na matarajio ya ulimwengu. Vivyo hivyo, mazingira ya nchini Kenya yanalazimu mawasiliano ya kimataifa kupitia mkakati wa msisitizo wa utulivu wa kisiasa, maendeleo ya uchumi, maendeleo ya jamii, mazingira endelevu na uvumbuzi wa kiteknolojia.

## 2.2 Wahusika katika Mandhari ya Sera ya Masuala ya Kigeni ya Kenya

Wahusika katika Sera ya Masuala ya Kigeni ya Kenya hujumuisha wahusika wa taifa na wasiokuwa wa taifa na pia wengine wasiokuwa wa asilia nchini. Hii inatokea kutokana na maagizo ya Katiba na vifaa vya sheria vinavyosisitiza ujumuishaji, utawala wazi na kuzingatia misimamo ya demokrasia. Hivyo, wahusika wafuatao wa kitaifa na wasio wa kitaiafa watakuwa miongoni mwa watakaotekeleza sera hii ya Masuala ya KIgeni:

a) Wananchi
b) Rais
c) Baraza la Mawaziri
d) Baraza la Usalama wa Taifa na Kamati ya Baraza la Usalama wa Taifa
e) Bunge
f) Mahakama
g) Serikali za Kaunti
h) Taalimu ya Huduma za Kigeni
i) Wakenya waishio nje ya nchi
j) Wasomi
k) Sekta ya Kibinafsi
l) Mashirika ya Kijamii
m) Vyombo vya Habari
n) Taasisi za Kidini
o) Wanawake
p) Vijana

q) Watu waishio na Ulemavu
r) Mashirika ya Wafanyikazi

## 2.3 Matumizi ya Diplomasia ya Umma

Kenya itaendeleza matumizi ya diplomasia ya umma kama uwenzo wa kusemezana na hadhira nchini na zile za kigeni kuimarisha mshikamano, kujenga uaminifu, na kuendeleza ushirikiano, na mwishowe kuanzisha mazingira ya ulimwengu yaliyo salama zaidi. Diplomasia ya Umma imejumuishwa kimakusudi katika mijadala inayohusisha mataifa mawili na ile ya mataifa mengi ili kuunga mkono malengo ya muda mrefu ya Sera ya Masuala ya Kigeni ya Kenya na kuendeleza matakwa ya Kenya kimataifa.

Mawasiliano lengwa yatashughulikiwa katika mkondo wa kutekeleza Sera hii ya masuala ya Kigeni ili kukuza uaminifu ya umma; kupata mwonekano, ufaafu, heshima na kuleta uwazi. Utekelezaji utashughulikiwa kwa wakati ufaao na kwa misingi ya mahitaji kupitia mawasiliano mseto na mkakati mpana wa mawasiliano hayo ambayo yatajumuisha vipindi vya majadiliano redioni na katika runinga, maoni, maandishi magazetini, maelezo, maelezo ya kidemokrasia yaliyopangwa, miongoni mwa mengine.



*Kuonyesha Kenya kwa Ulimwengu*

# *Sura* 3:

# DIPLOMASIA YA PANDE MBILI NA YA PANDE NYINGI

## 3.1 Ufafanuzi wa Ujirani wa Kidiplomasia wa Kenya

Kenya daima imefuata msimamo wa ujirani mwema kujichukulia imeunganishwa na majirani wake katika nyonga. Hii inamaanisha nchi yetu ni sehemu ya mtandao wa kimaeneo wa uhusiano na ushirikiano.

Uhusiano wa baina ya watu na mataifa mengine huanza na majirani,na hivyo, umuhimu wa kukuza ushirikiano wa eneo na umoja kwa manufaa ya pamoja. Jumuia ya Afrika Mashariki (EAC) na Halmashauri ya Serikali mseto juu ya Maendeleo (IGAD), ndizo nguzo za ustawi wa pamoja, amani na usalama wa eneo. Umoja wa kihistoria wa nchi ndugu ya Uganda, imebakia kuwa mshirika anayeongoza wa kibiashara na Kenya.

Majirani ni washirika muhimu kwa usalama, maendeleo, amani na usalama katika eneo. Kila nchi katika eneo imeneemeka na rasilimali asilia na mzuri wa eneo kimkakati, ambao ni wa manufaa katika kubadili uchumi wa kila nchi mshirika na kwa pamoja, kulifanya eneo la Afrika Mashariri kitovu cha biashara ya ulimwengu. Hata hivyo, Kenya na majirani wake iko karibu na njia muhimu za baharini kuanzia Bahari ya Shamu, Ghuba la Eden na Bahari ya Hindi. Kenya inapendekeza mkakati wa masuala ya bahari ya eneo kudhibiti matakwa ya eneo ya mkakati huu katika nyanja za uchumi wa kieneo na usalama wa siasa za eneo. Fauka ya haya, Kenya inapigania ongezeko la uunganisho wa miundo mbinu katika eneo, kuangama katika uzuri linganishi wa kila nchi.

## 3.2 Ushirika uwili na Mataifa ya Afrika

Kenya inachukulia bara la Afrika kama kiini cha umataifa. Kitambulisho cha Afrika kimo rohoni mwa sura ya Kenya ulimwenguni. Hivyo Kenya inaupa kipaumbele uhusiano wake na nchi za Afrika na inazingatia msimamo wa Uafrika na kuhakikisha kubaki msitari wa mbele kutetea maswala ya Afrika katika ulingo wa ulimwengu. Kenya imeanzisha misheni za kidiplomasia changamfu katika maeneo yote Matano ya bara la Afrika. Kenya inachukulia kwamba maeneo yote haya matano yana manufaa ya kipekee kwa malengo ya sera ya masuala ya kigeni ya nchi yetu.

Kenya pia imetimiza malengo ya Umoja wa Afrika ya kuondoa mipaka na viza (ruhusa ya kuzuru) kwa kuondoa masharti yote ya viza kwa mataifa yote ya Afrika. Nchi yetu iko msitari wa mbele kwa kuendeleza umoja wa Afrika kwa kufungua mipaka yake kwa Waafrika wengine kupitia sera inayoanzisha usafiri bila viza kwa wananchi wote wa Bara la Afrika na kwengineko.

Kenya inazingatia msimamo wa pamoja wa Umoja wa Afrika na mambo ya

ulimwengu yanayohusiana na msimamo wa kisiasa kimaeneo wa bara na dhima ya Umoja wa Afrika katika ushirikiano wa kimataifa, amani na usalama. Nchi yetu inaendelea kupigania umoja wa bara letu katika maendeleo, agenda ya mabadiliko ya tabianchi, pia amani na usalama. Inaendeleza biashara kati ya miongoni mwa mataifa na inaendelea kuunga mkono na kuendeleza maendele ya Maeneo huru ya Biashara ya Afrika (AICFTA) kwa manufaa kubaliano ya mataifa washiriki. Nchi yetu inatafuta Jumuia ya Afrika yenye nguvu na toshelezi ili kuendeleza na kutetetea matakwa ya pamoja ya bara nak ama maeneo mengine.

## 3.3 Uhusiano Uwili na Ulimwengu wote

Uhusiano wa Kenya na nchi zote ulimwenguni unajumuisha nchi za Asia na Pacific, Ulaya, Amerika na nchi za Carrebian, Mashariki ya Kati na Eneo la Magharibi mwa Bahari  Hindi.

## 3.4 Diplomasia inayohusisha Nchi Nyingi

Kenya imeanzisha sifa zake kama kiongozi wa suluhisho nyingi kwa matatizo ya ulimwengu na itazidisha kuchangia mpangilio wa nchi nyingi katika ugavi unaokubalika. Ushirikiano uliofaulu na mashirika ya kimataifa katika mikutano ya wahusika wengi imekuwa sifa kuu ya Sera ya Masuala ya Kigeni ya Kenya.

Ushiriki mchanagamfu wa Kenya katika mashirika ya maeneo na kimataifa kama vile Jumuia ya Afrika Mashariki (EAC), IGAD, COMESA, Umoja wa Afrika, OACPS na Umoja wa Mataifa (UN) unairuhusu kusukuma ushawishi mkubwa katika utulivu wa eneo na miundo ya utawali ya ulimwengu. Kwnya itaendelea kusukuma marekebisho ya taasisi za Umoja wa Afrika kuhakikisha Umoja wa Afrika unafadhiliwa kifedha na ulio na uwezo wa kukabiliana na changamoto za Bara na kuendeleza matakwa muhimu. Kenya pia ni mshirika mtendaji wa Shirika la Biashara Ulimwenguni (WTO); Shirika la Ulimwengu la Akili Mali (Intellectual Property) (WIPO) na Kongamano la Umoja wa Mataifa la Biashara na Maendeleo (UNCTAD).

Ushiriki huu tendi hauongezi tu sura ya Kenya kidiplomasia lakini pia unaenda sambamba na vipaumbele vya taifa na malengo ya maendeleo.




*Mchoro 1: Ushirikiano wa kidiplomasia wa Kenya*




*Picha ya: Baadhi ya Baba Waanzilishi wa Shirika la Umoja wa Afika (OAU)*

## 3.5: Sera ya Masuala ya Kigeni ya Kenya katika Ushirikiano wa Makundi Mengi

Kenya imekuwa mshirika wa makundi mengi ya ushirikiano kama vile Umoja wa Madola, NAM, G77 na China, na IQRA miongoni mwa mengine. Kenya imetumia uhusiano huu kuendeleza ajenda yetu, kuimarisha nafasi na masuala kama vile utawala wa bahari, mashauriano ya biashara na uchumi.

Sera hii inatambua kwamba ni kwa manufaa ya Kenya kufuatiliza, kuchanaganua na kuzungumza na washirika na makundi madogo madogo ulimwenguni kama jibu kwa mabadilikoya binadamu na ongezeko la vijana watakaohitaji nafasi za ajira, huduma za uwezo kimaendeleo, maisha bora, biashara na nafasi za uwekezaji.

## 3.6: Kubadilisha Nairobi kuwa Kitovu cha Ushirikiano na Huduma za Fedha

Nairobi imejitokeza kama kituo muhimu cha huduma za fedha na ushirikiano wingi kwa sababu ya mahali pazuri, pakijumuisha sekta ya benki sifika, ubadilishaji pesa unaonawiri, miundo msingi bora, uchumi mpana na rasilimali watu walio na stadi na waliosoma vizuri. Nairobi ni makao ya mashirika mengi ya kimataifa na Umoja wa Mataifa, fedha zao, programu zao, na vituo vyao. Ni makao makuu ya Programu ya Mazingira na Makao ya Umoja wa Mataifa, Kituo cha Huduma za Kibinadamu Ulimwenguni hivyo kuifanya kuwa kitofu faafu cha ushirikiano ulimwenguni. Ofisi ya Umoja wa Mataifa Nairobi, ndiyo Sekretarieti ya kazi pekee ya tatu kwa ukubwa na inahudumu kama Makao Makuu ya Umoja wa Mataifa barani Afrika na Kusini mwa Ulimwengu.Kama kituo cha fedha kinachoongoza katika eneo hili, ni makao ya Shirika la Fedha la KImataifa (IMF), Benki ya Maendeleo ya Afrika na kituo kikubwa zaidi cha Benki ya Ulimwengu nje ya Washington. Mtazamo wa sera hii, kwa hivyo unalenga kuendeleza Nairobi kama kituo kinachoongoza kiushirikiano na kifedha.

# *Sura* 4:

# SERA YA MASUALA YA KIGENI: MAENEO LENGWA

## 4.1 Maeneo Lengwa Manane

Kutokana na mashauriano mapana na ushirikiano na washikadau mbalimbali, maeneo lengwa manane yafuatayo yalifikiriwa na kukubalika kwamba ndiyo nguzo za Sera ya Masuala ya Kigeni ya Kenya:

i) Diplomasia ya Amani na Usalama
ii) Diplomasia ya Uchumi na Biashara
iii) Diplomasia ya Bahari na Umakinifu
iv) Diplomasia ya Utawala Ulimwenguni na Ushirikiano Mwingi
v) Diplomasia ya Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi
vi) Diplomasia ya Sayansi, Teknolojia na Uvumbuzi
vii) Diplomasia ya Wakenya wanaoishi nje ya Nchi; na
viii) Diplomasia ya Jamii na Utamaduni

*Mchoro 2: Muundo wa Sera ya Kigeni*




*Asili: SDFA*

## 4.2 Diplomasia ya Amani na Usalama

Lengo kuu la Kenya la Diplomasia ya Amani na Usalama ni kulinda uhuru wa Kenya na heshima ya mipaka yake, kudumisha demokrasia na haki muhimu za kibinadamu, na kuhakikisha ustawi na maisha bora ya Wakenya. Eneo lengwa hili limechota kimsingi,kutoka msimamo wa kudumisha amani na usalama wa kimataifa kama ilivyokitwa katika Mkataba wa Umoja wa Mataifa na kusisitizwa zaidi na Sheria ya Kikatiba ya Umoja wa Afrika; Mkataba wa Kuanzisha Jumuia ya Afrika Mashariki na mikataba mingine ya kimataifa,maelewano na makubaliano ya amani na usalama

*Mchoro 3: Kenya la Diplomasia ya Amani na Usalama*




*Asili: Wizara ya Ulinzi ya Kenya*

## 4.3 Diplomasia ya Kiuchumi na Biashara

Diplomasia ya Kiuchumi na Kibiashara ni sehemu muhimu ya Sera ya Masuala ya Kigeni ya Kenya. Jitihada za Kidiplomasia kwa hivyo zitaendelea kuenezwa ili kuendeleza ukuaji wa uchumi na maendeleo kupitia majadiliano yenye manufaa. Majadiliano haya yatalenga wahusika wa taifa na wasio wa taifa katika daraja za ushirikiano wa makundi mawili na ushirikiano unaojumuisha makundi mengi.

Kiini cha demokrasia ya Kenya ya Uchumi na Biashara, ni kuinua uwezo wa wanawake kiuchumi, vijana, wanaojiweza tofauti tofauti na makundi ya watu

wachache. Jitihada maalumu zitafanywa kusaidia na kuwezesha kufikia masoko ya nchi kimaeneo na kimataifa, na fedha za maendeleo. Katika eneo lengwa hili, kipaumbele kitapewa biashara na uwekezaji; teknolojia; Uchumi bunifu; utalii; uchumi makinifu; fedha za maendeleo; maendeleo shirikiano na mawasiliano ya wengi.

*Mchoro 4: Nafasi tofauti za Kenya Ulimwenguni (p.12)*




*Mchoro 5 : Idadi na Usawazishaji wa Biashara ya Kenya, 2013-2022 (KSh '000)*




Asili: Benki Kuu ya Kenya 2024

## 4.4 Diplomasia ya Bahari na Uchumi Makinifu

Bahari zinatapakaa ardhini kwa zaidi ya asilimia sabini (70%) na zina dhima muhimu sana katika masuala ya ulimwengu. Ni chanzo cha chakula, umeme, na usafiri, na zaidi ya asilimia tisini (90%) ya biashara ya ulimwengu hufanyika

baharini. Kwa upande mwingine, Kenya inamiliki uchumi makinifu mpana na sekta ya baharini ya nguvu, iliyo na uwezo wa kuchangia ukuaji wa uchumi na uzalishaji kazi, uthabiti wa chakula, usafiri wa baharini na uendelevu wa mazingira.

Maendeleo ya sekta hii, yananuia kuchunguza na kuendeleza rasilimali za baharini na maziwa yaliyo bora, kukinga maeneo na mipaka ya bahari, kukabiliana na tishio la bahari, kuongeza ushirikiano, kutumia maeneo ya bahari na pwani, kulinda mazingira ya baharini na kutoa vifaa na huduma kusaidia shughuli na faida za baharini na uvuvi. Inakusudia pia kuchangia ugavi sawa wa faida na rasilimali za bahari na uvuvi. Kenya itazidisha nafasi yaye kama kiongozi wa kimataifa wa bahari na uchumi makinifu na kuchangia kimaana juhudi za ulimwengu katika utawala wa bahari.

## 4.5 Diplomasia ya Utawala wa Ulimwengu na Uhusiano wa Mataifa mengi.

Sera ya Masuala ya Kigeni ya Kenya imejikita katika uhalisia wa ulimwengu ambao daima unabadilika, kuunganika zaidi na wa kutegemeana. Kutokana na mabadiliko haya, hujitokeza nafasi kadhaa, changamoto, tishio na hatari takribani kwa kiwango sawa. Hali hii inachangiwa na hali mbalimbali kama vile mabadiliko ya kisiasa kimaeneo, mashindano ya uwezo mkubwa na ongezeko lisiloisha la utaifa. Vichangio vingine vinatokana na kutoaminika kwa nguvukazi na mashindano ya vianzo vyake; tofauti za maendeleo ya kiuchumi; wingi wa wahusika katika ulingo wa ulimwengu; uchangamano na masuala mbalimabali yanayoshughulikiwa katika nchi moja; maendeleo ya teknolojia na uvumbuzi pamoja na biashara zao na matokeo hasi. Juu ya haya ni masuala mengine yanayosambaa mipakani na masuala ya pande zote mbili kama vile mabadiliko ya tabianchi; changamoto za afya ya umma; mitazamo mikali ya ghasia; ukosefu wa uthabiti wa kiuchumi; changamoto ya haki za kibinadamu; tatizo la wakimbizi; utafutaji wa haki katika jamii, elimu, viwango vya kazi, na ujumla wa maendeleo endelevu. Kama kiongozi wa sasa wa mabadiliko ya taasisi za Umoja wa Afrika, Kenya tumejitolea kuanzisha Umoja wa Afrika wenye uwezo kupitia utoaji wa fedha ili ukabiliane na changamoto za barani na kuendeleza mikakati ya manufaa. Pia, kujikita katika mfumo wa uongozi wa ulimwengu na ushirikiano wa mataifa mengi, imejitokeza kuwa muhimu zaidi katika juhudi za usalama wa kimataifa unaofaa kutokana na kwamba hakuna taifa lolote ambalo linaweza kukwepa au kutatua masuala haya peke yake.

## 4.6 Diplomasia ya Mazingira na Tabianchi

Kenya imebarikiwa kuwa na rasilimali tofauti tofauti za mimea, Wanyama na nyingine asili zinazosaidia riziki za mamilioni, uchumi na maendeleo endelevu. Kenya ni makao makuu ya Programu ya Mazingira ya Umoja wa Mataifa na Programu ya Makao ya Binadamu ya Umoja wa Mataifa vile vile. Pia ni makao ya

Ofisi ya Umoja wa Mataifa jijini Nairobi, makao ya kipekee kati ka maeneo ya kusini mwa ulimwengu. Kenya itaendelea kusaidia, kudhamini utendakazi usio na matatizo na kuendeleza kupanda daraja kwa ofisi hizi na kuzipa nguvu hapa Nairobi

*Mchoro 6: Kwa nini Kenya inang'aa Afrika*




*Asili: Wizara ya Uwekezaji, Biashara na Viwanda*

## 4.7 Diplomasia ya Sayansi, Teknolojia na Uvumbuzi

Kenya inatambua dhima muhimu ya Sayansi, Teknolojia na Uvumbuzi (STU) katika ajenda yake ya maendeleo ya taifa. Kuzingatia unyuzi huu, Kenya inajumuisha aina mbalimbali za Sayansi, Teknolojia na Uvumbuzi kwa lengo la kujenga mshikamano thabiti ambao utaiwezesha kufikia matakwa yake ya taifa na kuiweka nchi katika kiwango cha mshiriki mkuu katika usemezano wa teknolojia ulimwenguni. Lengo la STU linaakisi kujitolea kwa Kenya katika ushirikiano wa kimataifa na ushirika unaoazimia kuvuta uwekezaji muhimu na kuendeleza kubadilishana elimu ili kukabiliana na changamoto ulimwenguni.

Diplomasia ya Kenya ya STU ni uwenzo muhimu sana wa Sera ya Masuala ya Kigeni, kutumia majukwaa ya kidijitali na teknolojia inayoendelea kuimarisha mahusiano yake ya kimataifa na uwepo ulimwenguni. Kufuatia msimamo huu, mkakati wa Kenya wa muungano wa teknolojia ibuka na teknolojia ya kisasa kama vile Akili Zalishi (AI) na matumizi ya mitambo, uhalisia mpana, data kubwa, Vyombo vya Habari, mtandao wa mambo, teknolojia ya kidijitali, uhalisia wa matumizi ya kompyuta, usalama wa vituo vya mitandao, pesa za mitandaoni, teknolojia ya anga, teknolojia ya kupeleka pesa kupitia mitandaoni (blockchain technology), na majukwaa ya kiteknolojia ya fedha (FonTechs) yataimarisha nafasi ya nchi kimataifa; kuvutia uwekezaji muhimu na kuimarisha nafasi ya nchi kama kitovu cha teknolojia

## 4.8 Diplomasia ya Wakenya wanaoishi nje ya Nchi

Diplomasia ya Kenya juu ya Wakenya wanaoishi nje ya Kenya imejikita katika mpangilio wa dhana ambayo inalinda, inahusisha na kuwezesha jamii ya Wakenya nje ya Kenya kuongeza ustawi wao na ule wa nchi yetu Lengo ni kulinda, kushirikisha na kuwezesha kiuchumi Wakenya hao. Wakenya hawa kwa sasa hivi wanadhaniwa kuwa milioni nne (4). Namba hii inatarajiwa kuongezeka kwa kuwa Wakenya wengi wanasafiri ng'ambo kutafuta elimu, mafunzo, ajira na nafasi za uwekezaji miongoni mwa sababu nyingine. Sera hii itaongeza program na vichocheo kuhimiza uwekezaji wa Wakenya hao, na kuanzisha mpango wa kutambua mafanikio ya Wakenya hao wa nje ya nchi. Sera hii pia itawezesha usajili wa vyama vya Wakenya nje ya nchi na kuhakikisha kuna mawasiliano ya uwazi bila siri.

*Mchoro 7: Uletaji pesa wa Wakenya nje ya nchi*




*Asili: CBK.*

## 4.9 Diplomasia ya Jamii na Utamaduni

Diplomasia ya jamii na utamaduni inamaanisha matumizi ya utamaduni, mila za jamii, na maadili kama nyenzo za kujenga uhusiano, kuendeleza maelewano na kuathiri mataifa mengine. Inamaanisha mtagusano wa watu kwa watu ambao huwa kama njia ya uwezo laini kwa kuanzisha mazingira ulimwenguni yafaayo kwa kushauriana. Kiini cha Diplomasia ya Jamii na Utamaduni ya Kenya inajumuisha matumizi ya utamaduni na turathi ; michezo; elimu; na afya. Kenya itaendelea kuvuna nafasi hizi za kijamii na kitamaduni kuongeza nafasi yake katika ulingo wa kimataifa, hususan kupitia maendelezo maadili ya jamii, turathi za kitamaduni na ruzuku asili nyingine za kitaifa

*Sura* **5**:

# MPANGILIO WA TAASISI NA UTEKELEZAJI

## 5.1 Jukumu la Sekretariati ya Serikali

Sekretarieti ya Utaratibu wa Serikali Kuu (NGCS), kitengo kikuu cha uratibu wa kiufundi itachukuwa nafasi kuu katika kuratibu na kusimamia wakati wa utekelezaji wa Sera hii. Kwa jumla, kuna ofisi kadhaa, taasisi za umma na washika dau ambao ni muhimu katika utekelezaji wa sera hii kama ilivyoangaziwa katika jedwali hapa chini:

***Jedwali 1: Muhtasari wa majukumu ya taasisi tofauti tofauti na Wahusika katika Utekelezaji wa Sera ya Masuala ya Kigeni ya Kenya***

| Na. | Taasisi | Majukumu |
|---|---|---|
| 1 | **Wananchi** | Wananchi ndio wateja muhimu sana wa sera ya Masualaya Kigeni. Wanaathiri utunzi, utekelezaji, na pia kutoa maoni na mwelekeo wa mjadala wa Sera ya Masuala ya Kigeni ya Kenya. |
| 2 | **Rais** | Rais ndiye Balozi Mkuu na huelekeza utekelezaji wa serahii. Rais atatekeleza jukumu hili kama ilivyo katika Katiba, Ibara 132 2(e), 4(b) na 5. |
| 3 | **Baraza la Mawaziri** | Baraza la Mawaziri litapitisha na kuratibu Mkabala wa Serikali na Jamii yote katika utekelezaji wa Sera hii. |
| 4 | **Baraza la Usalama la Nchi na Kamati ya Usalama ya Nchi** | Baraza hili na Kamati hii zitaendelea kuchunga na kuongoza Sera ya Masuala ya Kigeni ya Kenya. |
| 5 | **Wizara ya Masuala ya Kigeni na Wakenya wanaoishi nje ya Nchi** | Wizara ina jukumu la kusimamia Sera ya Masuala ya Kigeni kwa mujibu wa agizo katika Katiba na Amri ya Rais Na. 2/2023. Wizara pia ina jukumu la kuonyesha, kuendeleza na kutetea matakwa na sura ya Kenya ulimwenguni. Wizara itasambaza na kuhamasisha umma juu ya yaliyomo na maono ya Sera hii ya Masuala ya Kigeni. |

| Na. | Taasisi | Majukumu |
|---|---|---|
| 6 | **Wizara/Idara na Mashirika** | MDAs zitahusishwa katika utekelezaji wa sera hii, ikijumuisha uhakikishaji wa kuingizwa maeneo lengwa katika Sera, mipango na programu. |
| 7 | **Taalimu ya Huduma za Kigeni** | Taalimu itaimarisha maendeleo ya rasilimali watu na uwezo wa huduma za kigeni na washikadau wengine kwa utekelezaji fanisi wa sera. |
| 8 | **Serikali za Kaunti** | Serikali za Kaunti zitafanya kazi kwa karibu na MFDA kuendeleza biashara na uwekezaji, utamaduni, utalii, ushirikiano wa miji ndugu na suluhisho la masuala ya mipaka. |
| 9 | **Bunge** | Bunge litatunga sheria kupitia uwezo wasera hii, kutungasheria ambazo zitastawisha sera hii ya masuala ya kigeni, kuidhinisha mikataba ya kimataifa na makubaliano. Bunge litatoa unyapara, likijumuisha kuchunguza Mabalozi. Kamati za Bunge husika zitakuwa kiunganishi kati ya MFDA na Bunge. |
| 10 | **Mahakama** | Mahakama itachukuwa jukumu muhimu katika utekelezaji wa sera ikijumuisha masuala yanayohusika nahukumu ya kimataifa, na yataiweka Taalimu ya Sheria ya Kenya kama kituo cha mazungumzo ya sheria. |
| 11 | **Taalimu** | Taalimu hii itatoa maono yatakayoongoza na utafiti, kuwezesha mazungumzo ya kitaaluma, na kuchangia katika kuendeleza mikakati iliyojikita katika Ushahidi. |
| 12 | **Sekta ya Kibinafsi** | Kama wahusika wakuu katika biashara, uwekezaji, na uvumbuzi, Sekta ya Kibinafsi itaendeleza manufaa ya kiuchumi ya Kenya ng'ambo kupitia ushirikiano, upanuzi wa soko, na kushabikia bidhaa na huduma za Kenya. |

| Na. | Taasisi | Majukumu |
|---|---|---|
| 13 | **Mashirika ya Jamii Raia** | Mashirika ya Jamii Raia yataibua uelewa na kuhamasisha mtazamo wa umma juu ya malengo ya sera ya masuala ya kigeni. Yatajiweka na msimamo wa nchi wa pamoja katika shughuli za kigeni katika mpangiliokazi wa 'mkabalawa jamii yote'. |
| 14 | **Taasisi za Kidini** | Taasisi za kidini zina jukumu muhimu katika utekelezaji wa sera kupitia mazungumzo ya dini mbalimbali kwa pamoja na kuunga mkono jitihada zilizoanzishwa na serikali. |
| 15 | **Jamii ya Wakenya nje ya nchi** | Wakenya nje ya nchi watazidisha ushirikiano wao katika nchi wanamoishi kuchangia maendeleo ya taifa. |
| 16 | **Vyombo vya Habari** | Vyombo vya Habari ndivyo kiungo ambacho hueleza wananchi juu ya matukio ulimwenguni yanayoathiri Sera ya Masuala ya Kigeni ya Kenya. |
| 17 | **Washirika wa Maendeleo/Eneo/ Mashirika ya Kimataifa** | Washirika wa pande mbili na wale wa pande nyingi wa Kenya watatoa usaidizi muhuimu katika utekelezaji wa sera. |
| 18 | **Wanawake** | Wanawake watahusishwa katika kuendeleza usawa na ujumuisho wa jinsia katika uhusiano wa kimataifa na kidiplomasia. Watashiriki katika utekelezaji wa Programu ya Wanawake katika Diplomasia inayolenga kukuza wanafunzi wanawake wadogo kwa kazi za kidiplomasia na kuwezesha wanawake kuchukuwa nafasi za juu katika misheni za Kidiplomasia za Kenya na Mashirika ya Kimataifa. |
| 19 | **Vijana** | Vijana watahusishwa kikamilifu katika utekelezaji wa sera hii kwa kuwezesha uwakilishi wao katika shughuli za kimataifa na kupitia mijadala mfululizo juu ya masuala ya kawaida. |
| 20 | **Watu waishio na ulemavu** | Watu walemavu watajumuishwa kikamilifu katika utekelezajiwa sera hii kwa kuwezesha uwakilishi wao katika shughuli za kimataifa na kupitia mjadala mfululizo juu ya masuala ya kawaida. |
| 21 | **Mashirika ya Wafanyikazi** | Makundi ya wafanyikazi yatafanya kazi kwa karibu na Wizara ya Masuala ya Kigeni na Wakenya wanaoishi nje ya nchi kuendeleza na kulinda haki za wafanyikazi kwa kuzingatia mpangiliokazi unaotolewa chini ya Shirika la KImataifa la Wafanyikazi (ILO) na shughuli za kimataifa za kazi. |

*Sura* **6**:

# USIMAMIZI NA UTATHMINI

## 6.1 Umuhimu wa Kupima Matokeo ya Kidiplomasia

Sera hii inatambuwa umuhimu wa kutathmini matokeo ya kidiplomasia na athari zake. Wizara itashirikiana na taasisi za elimu na makundi tafakuri kuunda nyenzo za kupima athari ili kutathmini matokeo ya sera hii. Uhakiki wa muhula wa kati na mwisho utafanyika kutathmini maendeleo ya usimamizi na kufikia malengo yanayodhamiriwa.

Mpangilio wa matokeo utaundwa kueleza vionyeshi mahususi vitakavyopima maendeleo ya matokeo na mianzo lengwa. Mpangilio huu utatowa utathmini iwapo juhudi zinazofanywa zinatoa matokeo yanayotarajiwa. Jambo hili litawezesha kufanya maamuzi yaliyo na Ushahidi na kuendeleza kusoma na kuboresha mfululizo wakati wa utekelezaji, hivyo kuwezesha urekebishaji kwa wakati ufaao wa mikakati kwa kutegemea changamoto na nafasi za kazi, uwekezaji na miradi.

Mkabala endelezi huu utahakikisha kwamba sera itakubali mabadiliko ya mfanyiko ulimwenguni huku ikibaki kuwa kiini cha Kwenda sambamba na vipaumbele vya taifa.

### 6.1.1 Mpangilio wa Kitaifa wa Usimamizi na Utathmini

Usimamizi na Utathmini wa Sera hii, utaongozwa na mpangiliokazi wa Kitaifa na Usimamizi ambao umekitwa katika Mfumo wa Taifa Mseto wa Kusimamia na Kutathmini (NIMES). Wizara inayohusika na Masuala ya Kigeni na Wakenya wanaoishi nchi za nje ya Kenya, itaratibu usimamizi na utathmini kuhakikisha kwamba malengo ya sera hii yametimizwa. Serikali pia itatumia nyenzo zilizopo, ikijumuisha MDAs, Mipangilio Mkakati, Mikataba ya Utendakazi ya kila Mwaka, Mipango ya kazi ya kila Mwaka, Ripoti ya Rais ya kila Mwaka ili kufuatilia utekelezaji na kutoa ripoti ya sera hii. Jambo hili pia, litafuata Mpangiliokazi wa wakati kadri. Kuongezea , Wizara ya Masuala ya Kigeni na Wakenya walio nje ya nchi, itatayarisha miongozo ya sura ya Sera ya Masuala ya Kigeni ya kila mwaka kuweka ajenda na vipaumbele kwa utekelezaji kila mwanzo wa mwaka. Fauka ya hayo, utekelezaji utafuatiliwa, utathminiwe, na kutolewa ripoti kila baada ya muda fulani ili kutathmini ufanisi wa malengo, kutambua mapengo na changamoto zinazokabili utekelezaji wake, na matendo sahihishi yanayohitajika kuhakikisha kufikia matokeo yanayotarajiwa.

Kwa jumla, Usimamizi na Utathmini utahitaji kujitolea kwa taasisi tekelezi zote kama inavyoelekezwa katika mpangokazi wa taasisi. Pia, Sera hii itapitiwa upya mahitaji yanapotokea ili kuingiza masuala ibuka katika mazingira ya nchini na ya nje ya nchi.

# ALAMA YA KIDPLOMASIA YA KENYA




## MISHENI ZA KIDIPLOMASIA

**KENYA**
1. The United Nations Environment Programme (UNEP)
2. The United Nations Human Settlements Programme (UN-HABITAT)

**AFRICA**
3. Abidjan
4. Abuja
5. Accra
6. Addis Ababa
7. Algiers
8. Bujumbura
9. Cairo
10. Dakar
11. Dar-Es-Salaam
12. Djibouti
13. Gaborone
14. Harare
15. Juba
16. Kampala
17. Khartoum
18. Kigali
19. Kinshasa
20. Luanda
21. Lusaka
22. Maputo
23. Mogadishu
24. Pretoria
25. Rabat
26. Windhoek

**AMERICAS AND THE CARIBBEAN**
27. Brasilia
28. Havana
29. New York
30. Ottawa
31. Washington D.C

**ASIA & PACIFIC**
32. Bangkok
33. Beijing
34. Canberra
35. Islamabad
36. Jakarta
37. Kuala Lumpur
38. New Delhi
39. Seoul
40. Tokyo

**EUROPE**
41. Ankara
42. Berlin
43. Bern
44. Brussels
45. Dublin
46. Geneva
47. London
48. Madrid
49. Moscow
50. Paris
51. Paris - The United Nations Educational, Scientific and Cultural Organization (UNESCO)
52. Rome
53. Stockholm
54 The Hague
55. Vienna

**MIDDLE EAST**
56. Abu Dhabi
57. Doha
58. Kuwait
59. Muscat
60. Riyadh
61. Tehran
62. Tel Aviv

## UBALOZI MDOGO

**AFRICA**
63. Goma

**AMERICAS**
64. Los Angeles
65. Port-au-Prince

**ASIA & PACIFIC**
66. Guangzhou

**MIDDLE EAST**
67. Dubai
68. Jeddah

## OFISI ZA URATIBU

**AFRICA**
69. Arusha
70. Hargeisa

**Note**: Kenya will continuously enhance its diplomatic footprint by progressively establishing new missions to strengthen its global presence and promote foreign policy objectives.


25


24


23


22


17


16


15


14


13


12


11


10


9


8


7


6


5


4


3


2


21


20


19


18

# Picha na majina ya Mawaziri wa Masuala Ya Kigeni

25. Mheshimiwa.Dkt. Musalia Mudavadi, EGH, Prime Cabinet Secretary & Waziri wa Masuala ya Kigeni na Mambo ya diaspora *( 2023 - kufikia sasa)*
24. Dkt. Alfred Mutua, Waziri wa Masuala ya Kigeni na Mambo ya Diaspora *(2022-2023)*
23. Amb. Raychelle Omamo, Waziri wa Masuala ya Kigeni *(2020-2022)*
22. Amb.Dr. Monica Juma, Waziri wa Masuala ya Kigeni *(2018-2020)*
21. Amb.Dr. Amina Mohammed, Waziri wa Masuala ya Kigeni na Biashara ya Kimataifa *(2013-2018)*
20. Amb.Prof. Samson Kegengo Ongeri,EGH., Waziri wa Masuala ya Kigeni *(2013)*
19. Mheshimiwa Mstahiki.Prof. George Museng Saitoti, EGH.,Ag. Waziri wa Masuala ya Kigeni *(2010-2012)*
18. Mheshimiwa. Moses Masika Wetangula, Waziri wa Masuala ya Kigeni *(2008-2012)*
17. Mheshimiwa Raphael Tuju, Waziri wa Masuala ya Kigeni *(2005-2007)*
16. Mheshimiwa Chirau Ali Mwakwere, Waziri wa Masuala ya Kigeni *(2004-2005)*
15. Mheshimiwa. Marsden Madoka, Waziri wa Masuala ya Kigeni *(1998-2001)*
14. Mheshimiwa. Christopher Mogere Obure, Waziri wa Masuala ya Kigeni *(2001)*
13. Mheshimiwa. Dr.Bonaya Adhi Godana, Waziri wa Masuala ya Kigeni *(1998-2001)*
12. Mheshimiwa Mstahiki. Stephen Kalonzo Musyoka, EGH, Waziri wa Masuala ya Kigeni *(1993-1988) & (2003-2004)*
11. Mheshimiwa, Wilson Ndolo Ayah, Waziri wa Masuala ya Kigeni *(1990-1993)*
10. Mheshimiwa. Dkt. Zachary Onyonka, Waziri wa Masuala ya Kigeni *(1987-1988)*
9. Mheshimiwa. Elijah Wasike Mwangale, Waziri wa Masuala ya Kigeni *(1983-1987)*
8. Dkt. Robert Ouko, Waziri wa Masuala ya Kigeni *(1979-1983) & (1988-1990)*
7. Mheshimiwa.Munyua Waiyaki, Waziri wa Masuala ya Kigeni *(1974-1979)*
6. Mheshimiwa.Magana Njoroge Muigai, Waziri wa Masuala ya Kigeni *(1969-1974)*
5. Mheshimiwa.Peter Mbiyu Koinange, Waziri wa Masuala ya Kigeni *(1969)*
4. Mheshimiwa. Arwings Kodhek, Waziri wa Masuala ya Kigeni *(1968-1969)*
3. Mheshimiwa. James Nyamweya, Waziri wa Masuala ya Kigeni *(1967-1968)*
2. Mheshimiwa.Joseph Murumbi, Waziri wa Masuala ya Kigeni *(1964-1966)*
1. Mheshimiwa Mstahiki. Jomo Kenyatta,Waziri wa Masuala ya Kigeni *(1963-1964)*


1



JAMUHURI YA KENYA

MAWASILIANO:

Jumba la zamani la Hazina
Baraste ya Harambee

NAMBARI ZA SIMU:
+254 20 3318888
+254 020 494900
0710 600978
0733 318 868

BARUA PEPE:
info@mfa.go.ke